



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO

Unapojibu tafadhali taja

**Kumb Na.:** HWB/F.10/175/163

Tarehe: 07 Disemba, 2023

Watumishi wote,  
Halmashauri ya Wilaya,  
S.L.P. 59,  
**BAGAMOYO.**

**TANGAZO LA MKOPO KWA WATUMISHI WA UMMA HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO  
KWA MWEZI DISEMBA, 2023 TSHS. 350,000,000/=**

Kichwa cha habari hapo juu chahusika.

2. Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo imepokea fedha jumla ya **Tshs. 350,000,000/=** kutoka Wizara ya fedha na Mipango ikiwa ni mwendelezo wa mikopo inayoletwa kwa watumishi wa Umma, kwa kuzingatia waraka wenye **Kumb. Na. C/AC.7/228/01/16** wa tarehe **30 Juni, 2011** kuhusu utaratibu wa kukopesha fedha taslimu watumishi wa Serikali kwa ajili ya kununua magari, pikipiki, samani na matengenezo ya magari na pikipiki, aidha kwa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo fedha hizi ni za awamu ya nne (4).

3. Kwa tangazo hili, mnajulishwa kwamba mnatakiwa kuwasilisha maombi yenu ya mkopo husika katika Mfumo wa Mikopo ya Hazina unaoitwa "**Hazina Portal**" kupitia kujisajili kwenye link "**als.muse.go.tz**" ili uweze kutengeneza akaunti na kuapply mkopo wako si zaidi ya tarehe **22 Disemba, 2023** saa **9:30** alasiri. Kwa msaada wa usajili, wasiliana na wataalam wafuatao:-

- |                   |                             |               |
|-------------------|-----------------------------|---------------|
| 1) Nawile Maokola | - Afisa Utumishi Mwandamizi | 0713 42 36 99 |
| 2) Podius Gosbert | - Afisa Tehama              | 0787 25 51 43 |

Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)

fisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo, Barabara ya Uhindini, S.L.P. 59, 61301 BAGAMOYO Mkoa wa Pwani.  
Simu Na: 0733 860 575, Nukushi: 023 2440338 Barua Pepe: [ded.bagamoyo@pwani.go.tz](mailto:ded.bagamoyo@pwani.go.tz). Tovuti: [www.bagamoyodc.go.tz](http://www.bagamoyodc.go.tz)

4. Aidha taarifa utakazoingizwa wakati utakapojisajiri katika link tajwa hapo juu ziwe sawa sawa na taarifa zako zilizopo katika Mfumo wa taarifa za Mishahara yaani **"NEW HCMIS"**
5. Masharti na vigezo vya mkopo vinavyohitajika ni kama ifuatavyo:-
  - i. Lazima awe Mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo.
  - ii. Mshahara wake usipungue **1/3 "Basic Salary"**
  - iii. Awe tayari kukatwa makato ya mkopo kupitia mshahara wake.
  - iv. Awe tayari kujaza mkataba utakaotoka kwenye mfumo wa **"Hazina Portal"**.
  - v. Kiwango cha mkopo kitakachotolewa ni kila kitakachokuwa kimeidhinishwa na kamati ya mikopo itakayokuwa imeundwa na Mkurugenzi Mtendaji.
  - vi. Asiwe mnufaika mkopo iliyotolewa miaka ya **2020, 2021** na **2022** kama hajamaliza kurejesha mikopo hiyo.
  - vii. Maombi ya mikopo yazingatie aina ya mkopo na viwango vilivyoainishwa katika jedwali
6. Jedwali lenye mchanganuo wa mkopo limeambatishwa.
7. Nawatakia kazi njema.



Majid S. Mhina

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
BAGAMOYO.**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA WILAYA  
BAGAMOYO**

**NB: Tangazo hili pia linapatikana kwenye website ya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ambayo ni [www.bagamoyodc.go.tz](http://www.bagamoyodc.go.tz)**

NBM-UTUMISHI

Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo, Barabara ya Uhindini, S.L.P. 59, 61301 BAGAMOYO Mkoa wa Pwani.  
Simu Na: 0733 860 575, Nukushi: 023 2440338 Barua Pepe: [ded.bagamoyo@pwani.go.tz](mailto:ded.bagamoyo@pwani.go.tz). Tovuti: [www.bagamoyodc.go.tz](http://www.bagamoyodc.go.tz)

VIWANGO VIPYA VYA MIKOPO YA FEDHA TASLIM

NA	AINA YA MIKOPO	NGAZI YA MSHAHARA	KIWANGO CHA JUU CHA MIKOPO KINACHOPENDEKEZWA (TSHS)	MUDA WA MAREJESHO
1	Mkopo wa fedha taslimu kwa ajili ya ununuzi wa magari, pikipiki, samani na matengenezo ya vyombo vya usafiri	TGS A-C, TGTS A-C, TGHS A-C AGCS 1-2, TGHOS A-C, SAIS A-C TGS D-F, TGTS D-F, TGHS D-F, AGCS 3-4, TJS 3-5, TGRS A-C, SAIS D-F TGS G-H, TGTS G-H, TGHS G-H, AGCS 5-6, TJS 6, TGRS D-E, SAIS G-H LSSE 1-4, TGTS I, TGHS I-J AGCS 7-9, TJS 7-9, TGRS F-I, SAIS I-K LSSE 5-9, TGHS K-L, AGCS 10-12, TJS 10-12, SAIS L-Q	15,000,000/=	Miezi 72
			30,000,000/=	Miezi 72
			40,000,000/=	Miezi 72
			50,000,000/=	Miezi 72
			55,000,000/=	Miezi 72